

MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

Tarehe 10/04/2024 kuingia na tarehe 09/04/2025 kutoka

Ndugu BANKI MOTORS BUILDING ambaye katika mkataba huu atajulikana kama (Mwenye Nyumba) anampangisha Ndugu BF-GHAT LIMITED ambaye katika mkataba huu atajulikana kama (Mpangaji)

Mashari ya Mkataba huu.

1. Nampangisha ndugu mtajwa hapo juu kwa gharama ya Tshs 1,200,000 ikiwa ni kiasi cha Tshs 1,200,000 kwa mwezi.
2. Umeme atanunua kwa zamu kwa kuachiana na wapangaji wanaochangia mita.
3. Mpangaji atachangia kiasi cha pesa ya malipo ya Maji kulingana na Bili itakapoletwa kwa mwezi kugawanya kwa wapangaji wote.
4. Mpangaji atatoa taarifa mwezi mmoja kabla endapo anataka kuhama kwa mwenye nyumba.
5. Mpangaji atapaswa kutumia nyumba/chumba kwa kuishi na familia yake tu.
6. Kelele zisizo za lazima hazitakiwi za kukela wapangaji wengine.
7. Siku ya kuondoka mpangaji utakabidhi nyumba/chumba kama ulivyokikuta ila kama kuna uharibifu wa aidha mlango, madirisha, vitasa/kitasa, kuchora kuta ama nyufa basi itabidi UKARABATI ndipo ukabidhi chumba/nyumba.
8. Ukarabati wowote utafanyika na mwenye nyumba au na mpangaji kwa makubaliano na mwenye nyumba.
9. Mpangaji akivunja mkataba wake mwenyewe hatorudishiwa pesa zake.
10. Gharama za kuvuta maji taka ni za wapangaji wenyewe (shimo likijaa mtachangia wote na kuita gari ije kuvuta maji taka).
11. Siku ya kuhama unatakiwa kukabidhi kwa mwenye nyumba funguo sawa na idadi uliyopewa siku unaingia kwenye chumba/nyumba.

Pande zote mbili zimetia saini mkataba huu kama ifuatavyo:

1. Saini ya Mwenye Nyumba [Signature] Tarehe 10/04/2024
Simu _____
2. Saini ya Shahidi wa mwenye Nyumba _____ Tarehe _____
Simu _____
3. Saini ya Mpangaji [Signature] Tarehe 10/04/2024
Simu 0715 123 501
4. Saini ya Shahidi wa Mpangaji _____ Tarehe _____
Simu _____